**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

Simu Na: +255 737 959 943
**"AFYA"**
E-mail : barua@manyararrh.go.tz
Website: www.manyararrh.go.tz

Hospitali ya Mkoa Manyara,
S.L.P. 577,
**BABATI.**

Unapojibu tafadhali taja:-

**TANGAZO LA NAFASI ZA KUJITOLEA**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara, kupitia Wizara ya Afya inatangaza nafasi za kujitolea kwa kada zifuatazo:-

**1. AFISA MUUGUZI DARAJA LA II NAFASI (3)**

**Sifa za Mwombaji:-**

a) Mwombaji awe na Shahada ya Uuguzi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
b) Awe amesajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania (TNMC)

**KAZI ZA KUFANYA**

i. Kutoa huduma za Kiuguzi
ii. Kukusanya takwimu muhimu za afya.
iii. Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
iv. Kuelimisha wagonjwa na jamii.
v. Kutoa huduma za kinga na uzazi
vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

**2. AFISA MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA LA II NAFASI (8)**

**Sifa za Mwombaji:-**

a) Mwombaji awe na Stashahada (Diploma) ya Uuguzi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
b) Awe amesajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania(TNMC)

**KAZI ZA KUFANYA**

vii. Kutoa huduma za uuguzi
viii. Kukusanya takwimu muhimu za afya.
ix. Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
x. Kuelimisha wagonjwa na jamii
xi. Kutoa huduma za kinga na uzazi
xii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

04/09/2024

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA
P.O.BOX 577
BABATI-MANYARA

3. **MSAIDIZI WA AFYA NAFASI (3)**

**Sifa za Mwombaji:**

Mwombaji awe amehitimu kidato cha nne na amepata mafunzo ya mwaka mmoja katika fani ya afya, ngazi ya afya ya jamii katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na amepata cheti cha **NACTE.**

**KAZI ZA KUFANYA**

- Kufanya usafi wa vifaa vya kazi, usafi wa wodi na mazingira
- Kusaidia wagonjwa wenye ulemavu na wasiojiweza
- Kumsaidia kumlisha mgonjwa asiyejiweza
- Kuchukua nguo za mgonjwa kuzipeleka kwenda kufuliwa
- Kuchukua sampuli za mgonjwa kwa ajili ya vipimo vya maabara na kufuatilia majibu
- Kutayarisha vifaa kwa ajili ya kusafisha na kufunga majeraha
- Kufuatilia mahitaji ya dawa kwa wagonjwa kutoka hifadhi ya dawa.
- Kufanya shughuli nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi.

4. **MHUDUMU WA CHUMBA CHA KUHIFADHI MAITI NAFASI (2)**

**Sifa za Mwombaji:**

Mwombaji awe amehitimu kidato cha nne na amepata mafunzo ya mwaka mmoja katika fani ya afya, ngazi ya afya ya jamii katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na amepata cheti cha **NACTE.**

**KAZI ZA KUFANYA**

- Kufanya usafi wa vifaa vya kazi, usafi wa wodi na mazingira
- Kusaidia wagonjwa wenye ulemavu na wasiojiweza
- Kumsaidia kumlisha mgonjwa asiyejiweza
- Kuchukua nguo za mgonjwa kuzipeleka kwenda kufuliwa
- Kuchukua sampuli za mgonjwa kwa ajili ya vipimo vya maabara na kufuatilia majibu
- Kutayarisha vifaa kwa ajili ya kusafisha na kufunga majeraha
- Kufuatilia mahitaji ya dawa kwa wagonjwa kutoka hifadhi ya dawa.
- Kufanya shughuli nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi.

5. **MTEKNOLOJIA DAWA NAFASI (5)**

**Sifa za Mwombaji:**

Mwombaji awe na Stashahada katika fani ya Uteknolojia dawa katika chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

04/09/2024



MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA
P.O.BOX 577
BABATI-MANYARA

**KAZI ZA KUFANYA**

- Kuainisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi.
- Kugawa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na watumishi
- Kuchanganya dawa
- Kuhifadhi dawa na vifaa tiba
- Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa
- Kukagua dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi katika eneo lake la kazi
- Kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa.
- Kuratibu kazi za kamati ya dawa ya hospital
- Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
- Kufanya uchunguzi wa ubora wa dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi
- Kufanya kaguzi mbalimbali katika sehemu zinazohifadhi dawa.
- Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
- Kufanya shughuli nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi.

**6. MTEKNOLOJIA MAABARA DARAJA LA II NAFASI (4)**

**Sifa za Mwombaji:**

Mwombaji awe na Stashahada katika fani ya Uteknolojia Maabara kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali pamoja na kuwa na Leseni

**KAZI ZA KUFANYA**

- Kupima Sampuli zinazoletwa Maabara.
- Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa Maabara za ngazi za juu.
- Kufanya kazi za ukaguzi wa Maabara, vitendanishi, vifaa, kemikali na hifadhi ya kemikali
- Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi.
- Kufundisha watumishi walio chini yake.
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

04/09/2024



MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA
P.O.BOX 577
BABATI-MANYARA

## 7. AFISA USTAWI WA JAMII DARAJA LA II (NAFASI 1)

**Sifa za Mwombaji:**
Mwombaji awe na Shahada ya Juu ya Ustawi wa Jamii (Social Work or Sociology) kutoka Chuo cha Elimu ya Juu kinachotambuliwa na Serikali.

**KAZI ZA KUFANYA**

**Zifuatazo ni huduma zinazotolewa na kitengo cha Ustawi wa Jamii (specific hospitali)**

- Kufanya uchunguzi wa kijamii na kutoa msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo na wale walio kwenye makundi hatarishi
- Kutoa ushauri wa kisaikolojia kwa wagonjwa/ndugu wa wagonjwa na watumishi wenye matatizo ya kijamii au kisaikolojia
- Kuhudhuria kliniki ya uangalizi na matibabu ya UKIMWI (CTC) na kutoa ushauri kwa wagonjwa kwa wale watakaobainika kuwa na matatizo ya kijamii ambayo hupelekea kuwa wafuasi wazuri wa dawa
- Kuhudhuria social ward rounds ili kugundua wagonjwa watakaohitaji huduma ya ki ustawi
- Kushughulikia mashauri ya ukatili wa jinsia na ukatili dhidi ya watoto
- Kushirikiana na vitengo vingine katika shughuli za uchangiaji damu
- Kuwaunganisha wagonjwa na vyanzo vingine vya huduma nje ya hospitali
- Kuwaunganisha wagonjwa na familia zao
- Kushughulika na wagonjwa waliotelekezwa wakiwemo watoto wachanga
- Kushuguhulikia mashauri mengine ya kijamii kwa kadiri yatakavyoibuka
- Kutoa elimu ya afya kwenye jamii kwaajili ya kuleta uelewa juu ya masuala mbalimbali yahusuyo afya.
- Kufanya supportive supervision kwa vituo vya afya.
- Kushughulikia mrejesho wa huduma (maoni, malalamiko, Pongezi na maulizo mbalimbali ya wagonjwa).

04/09/2024

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA
P.O.BOX 577
BABATI-MANYARA

8. **AFISA HABARI DARAJA LA II (INFORMATION OFFICER GRADE II) NAFASI (1)**

**Sifa za kuajiriwa:**

a) Mwombaji awe na cheti cha ufaulu kidato cha nne
b) Awe na cheti cha ufaulu taaluma/kada kwa ngazi ya Shahada
c) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
d) Awe na uwezo kufanya kazi za kuboresha mahusiano ya Taasis na ukuzaji wa huduma zitolewazo hospitalini

**KAZI ZA KUFANYA**

- Kukusanya na kuandika Habari zinazohusu Taasisi
- Kupiga picha na kuhifadhi kwa matumizi sahihi ya Taasisi
- Kuandaa habari kwa njia ya video kwa ajili ya kuitangaza Hospitali
- Kuandaa majarida , vipeperushi na mabango (Posters) kwa ajili ya kutangaza huduma zitolewazo Hospitalini
- Kukusanya takwimu mbalimbali katika matukio ya kuitangaza Hospitali
- Kutoa taarifa mbalimbali kuhusu fursa, Kampeni pamoja na matibabu mbalimbali yanayotolewa Hospitalini.
- Kushughulikia maswali,maoni na malalamiko kutoka kwa umma , waandishi wa habari, mashirika na wadau mbalimbali wa Hospitali.
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi

9. **FUNDI SANIFU VIFAA TIBA DARAJA LA II NAFASI (2)**

**Sifa za kuajiriwa:**

(a) Mwombaji awe na cheti cha ufaulu kidato cha nne
(b) Awe na cheti cha ufaulu taaluma/kada kwa ngazi ya Shahada ya Ufundi kutoka katika chuo kinachotambuliwa nanserikali
(c) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45

**KAZI ZA KUFANYA**

- Kufanya matengenezo ya vifaa vya huduma za tiba katika Hospitali ya Mkoa
- Kutunza kumbukumbu za kazi za kila siku
- Kushiriki katika kuagiza vifaa na vipuli vya kutengenezea vifaa Tiba vya hospitali
- Kutunza vifaa Tiba na vipuri
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

04/09/2024

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA
P.O.BOX 577
BABATI-MANYARA

## 10. AFISA TEHAMA DARAJA LA II NAFASI (1)

**Sifa za kuajiriwa:**

a) Mwombaji awe na cheti cha ufaulu kidato cha nne
b) Mwombaji awe na shahada ya Kompyuta katika moja ya fani zifuatazo; Sayansi ya Kompyuta, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Menejimenti ya Mifumo ya Habari au mafunzo mengine yanayohusiana na fani hii; kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.
c) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 4

**KAZI ZA KUFANYA**

- Kuandaa na kufanya majaribio ya tovuti na media anuai (Develop and test web pages and multimedia content)
- Kuboresha tovuti na media anuai (Update web pages and multimedia)
- Kuweka na Kuhakikisha usalama wa wovuti na medianuai (Lnplernent security for web pages and multimedia content)
- Kutoa huduma bora za kitaalam kwa watumiaji wa Tovuti na media anuai (Provide quality customer service)
- Kuratibu uwekaji wa taarifa za wavuti na medianuai kwa rnujibu wa sera husika (Publishing information in the web as per governing policy)
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA
P.O.BOX 577
BABATI-MANYARA
04/09/2024

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA WAOMBAJI WOTE**

i. Mwombaji awe ni Raia wa Tanzania
ii. Mwombaji awe na cheti cha ufaulu kidato cha nne
iii. Barua zote za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya kuhitimu elimu, taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha za rangi mbili za hivi karibuni (passport size)
iv. Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi (CV)
v. Mwombaji awe na ujuzi wa kutumia kompyuta (MS Excel & MS Word)
vi. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
vii. Testimonials result slips HAIZITAKUBALIWA
viii. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia ya makosa ya jinai mahakamani na kufungwa
ix. Nakala zote za vyeti zithibitishwe na mwanasheria

(*Uzoefu katika taaluma/kada husika atapewa kipaumbele*)

Mwombaji atume maombi kwa njia ya posta au kuwasilisha Ofisi ya Mganga Mfawidhi kabla ya tarehe 04.10.2024 saa 9:30 Alasiri katika anuani ifuatayo:-

**MGANGA MFAWIDHI,**
**HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA MANYARA,**
**S.L.P. 577,**
**MANYARA.**

Tangazo hili limetolewa tarehe 04.09.2024.

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA
P.O.BOX 577
BABATI-MANYARA

*Dkt. Katherine T. Magali*
**MGANGA MFAWIDHI**